AFRICAN UNION UNION AFRICAINE

الاتحاد الأفريقي UNIÃO AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: 251115517700/251115526373
Fax:251115518718/251115536950 Website: www.au.int

# Kiolezo cha Wasifu Kazi wa Nafasi ya juu ya Uongozi

| **Nafasi ya Kazi:** *(Onesha jina la nafasi ya kazi unayoomba)* |
|---|
| **MWENYEKITI WA TUME YA MUUNGANO WA AFRIKA** |

| **Taarifa Binafsi:** | |
|---|---|
| **Jina:** | **Mstahiki Mheshimiwa Raila Amolo Odinga, EGH** |
| **Anwani:** | Capitol Hill Square, 4th Floor Wing B, Upper Hill, Nairobi, Kenya |
| **Barua Pepe:** | amoloraila@gmail.com |
| **Namba ya Simu:** | +254 721 233 435 |
| **Tarehe ya Kuzaliwa (tarehe/mwezi/mwaka):** | 07/01/1945 |
| **Utaifa:** | MKENYA |
| **Uraia:** | MKENYA |
| **Jinsia:** | MWANAMUME |

**Dira ya Kazi** *(Kwa maneno yasiyozidi elfu moja (1000), elezea jinsi gani unakusudia kufikia matarajio yaliyoainishwa kwenye Ajenda 2063 na kushughulikia masuala muhimu zaidi yanayoikabili Afrika na Kamisheni katika kazi hii)*

Kama mwenyekiti wa Tume ya Muungano wa Afrika (AUC), nikiongozwa na falsafa ya uanaafrika na mwamko mpya wa Afrika, nitahakikisha nimetimiza azma na vipaumbele vya nchi wanachama wa muungano wa Afrika (AU). Uongozi wangu utakuwa wenye maono, wenye mageuzi, na wa kimatendo ili kutia kasi utekelezwaji wa matarajio ya wa Waafrika, malengo, na mipangilio ya ajenda 2063. Lengo na jukumu langu kuu ni kutumia kikamilifu rasilimali watu na maliasili tele tuliyonayo kuipa bara la Afrika ushawishi unaostahili ulimwenguni.

Kuafikia maono haya na kuelekeza Afrika mwamko mpya wa maendeleo ya pamoja, nitatekeleza malengo yafuatayo ya ajenda 2063:

1. **UanaAfrika, kupitia Ushirikiano na ujenzi wa Miundomsingi:** Hisia zangu za kimsingi kuhusu haja ya kujitambulisha na tamaduni zetu za Afrika na kujitolea kwa harakati za uanaAfrika ndio nguzo kuu katika filosofia yangu ya kisiasa. Nikiwa Mwakilishi Mkuu wa bara la Afrika katika masuala ya miundomsingi (2018 -2023), nilishuhudia manufaa ya kuwepo kwa umoja na mshikamano na vilevile nilishuhudia madhara ya utengano wa kikanda. Nitaharakisha Mpango wa Maendeleo ya Miundomsingi barani Africa (PIDA) ambao utasaidia katika kuleta

mshikamano katika bara letu. Mpango huu wa PIDA unahusisha kuwepo kwa barabara, mfumo wa ukuzaji wa maji, habari, miundomsingi ya mawasiliano na teknolojia. Licha ya kuwa na uwezo, miundomsingi katika bara la Afrika imedumaa na kukosa ufadhili wa kutosha. Nitaharakisha utekelezwaji wa PIDA kwa kutilia mkazo matumizi ya rasilimali asili za Afrika, kupitia ushirikiano kati ya umma na wawekezaji wa kibinafsi na maendeleo yanayoelekezwa na sekta ya kibinafsi ili kuunga mkono biashara huru katika bara la Afrika (AfCFTA).

2. **Maendeleo ya kiuchumi, ukuaji wa pamoja, na maendeleo endelevu:** Ili Afrika iweze kufikia uwezo wake wa juu kimaendeleo na kuwa na usemi katika mustakabali wa uchumi na biashara za dunia, itahija Afrika izingatie uongozi ambao utaweza kusimamia ipasavyo rasilimali zake za kiasili na kibinadamu. Nitatafuta njia za kutokomeza mbinu kandamizi katika biashara, kutatua mzigo wa madeni, kupigania uwekezaji katika elimu ya vijana na umma, kupigania uboreshaji wa wafrika katika masuala ya sayansi, teknolojia, maendeleo ya uvumbuzi na kujenga miungano ya kiuchumi itakayozingatia uzalishaji wa bidhaa barani Afrika na uuzaji katika mataifa ya nje pamoja na kuunga mkono ujasiriamali barani Afrika.

3. **Afrika yenye amani, demokrasia na usalama:** Bara la Afrika sharti liongoze katika kuendeleza utawala bora, demokrasia, usawa wa kijinsia, usawa, haki, uzingatiaji wa haki za kibinadamu na sheria. Ili kutimiza ajenda ya 2063, bara la Afrika linahitaji mikakati kabambe ili kukabiliana na chanzo cha migogoro, kuimarisha utekelezwaji wa sheria, kuunda taasisi zenye kufanya kazi na kuendeleza utawala bora. Nitafanya kazi na nchi wanachama wa Muungano wa Afrika, Mashirika ya Muungano wa Afrika na Jumuiya za Kikanda kukuza amani na usalama barani na kutatua changamoto zinazoibuka hasa ugaidi, uhalifu wa kupita mipaka Pamoja na uhalifu wa kimitandao.

4. **Kuimarisha Biashara ya Ndani kwa ndani baina ya mataifa ya Afrika:** Biashara ya ndani kwa ndani barani Afrika ni ya kiwango cha chini ikilinganishwa na mabara mengine yote. Eneo la Biashara Huru la Bara la Afrika (AfCFTA) ni nafasi ya kuunda soko la pamoja na kufanya biashara huru ndani ya bara, ili kutumia uwezo wake wa kiuchumi kikamilifu. Kwa utekelezaji mzuri wa AfCFTA, nitashirikiana na viongozi wa Afrika ili kuoanisha na kutekeleza sera za biashara katika ngazi za kitaifa, kikanda, kimataifa na kimataifa. Nitapigania mfumo wa biashara wenye haki na kuhimiza kuondolewa kwa vizuizi vya kibiashara ili kusukuma upatikanaji wa masoko, biashara ya bidhaa zenye thamani ya juu, na kuendeleza miundombinu. Nitaongoza harakati za kuwezesha uhuru wa kutembea kwa watu kote barani ili kuimarisha biashara ya ndani kwa ndani barani Afrika na uwekezaji, ikiwemo kuunda nafasi za ajira kwa vijana wa Afrika.

5. **Kuhimili makali ya Mabadiliko ya Tabianchi:** Ili kushughulikia tishio la mabadiliko mabaya ya tabianchi, ni muhimu kutambua athari zake mbaya kwa maendeleo ya Afrika. Licha ya mchango mdogo wa Afrika katika uzalishaji wa hewa chafu duniani, inaathirika kwa kiwango kikubwa kutokana na athari za uzalishaji wa gesi chafu. Hii inaleta gharama kubwa na kuelekeza rasilimali kutoka kwa mipango muhimu ya maendeleo hadi kwa mipango ya kushughulikia janga hili. Uongozi wangu utaweka kipaumbele juhudi za kurekebisha mabadiliko ya tabianchi ambayo ni za kuzuia, kubadilika, na zinazosaidia na kulinda miundombinu muhimu. Nitashinikiza nafasi kuu ya Afrika katika mipango ya kimataifa ya kuchukua hatua dhidi ya mabadiliko ya tabianchi ikijumuisha marekebisho, kupunguza na kujenga uwezo wa kuhimili hali mbaya kwa kutumia sayansi ya tabianchi. Nitaazimia kupigania fidia ya haki na kuongoza mikakati kamili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa nia ya kuhifadhi bioanuwai ya Afrika, misitu, ardhi, maji, maisha ya baharini na usalama wa mazingira.

6. **Usawa wa Kijinsia, Usawa na Uwezeshaji wa Vijana:** Wananchi wa Afrika, hasa wasichana, wanawake na vijana, ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya bara hili. Wakati sehemu nyingine za dunia zinakumbwa na kupungua na kuzeeka kwa idadi ya watu, idadi ya vijana wa Afrika inabakia kuwa faida ya kulinganisha sio tu kwa kuendesha ukuaji wa Afrika, bali pia kuziba pengo la utajiri duniani. Kutambua uwezo kamili wa Afrika kunategemea utekelezaji wa hatua za pamoja na za kibinafsi za kuwawezesha wasichana, wanawake na vijana kama vichocheo muhimu vya ubunifu na ukuaji. Nitapigia debe mikakati jumuishi ambayo hutoa fursa endelevu katika makundi mbalimbali ya watu wa Afrika.

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: 251115517700/251115526373
Fax:251115518718/251115536950 Website: www.au.int

**7. Utawala Bora:** Msingi wa amani, utulivu na ustawi wa Afrika lazima uwe katika utawala bora na taasisi imara ambazo zinakuza uwazi na uwajibikaji. Nimejitolea kufanya kazi na Mataifa Wanachama, Mashirika ya Muungano wa Afrika na Jumuiya za Kikanda katika kuendeleza utawala bora barani.

**8. Ushirikiano wa kimkakati**: Bara la Afrika lazima litekeleze jukumu kuu katika ulimwengu wa sasa wa utandawazi. Sitachoka kupigania vipaumbele na azma za bara la Afrika huku nikijenga ushirikiano mpya na kuimarisha ushirikiano uliopo. Ushirikiano wote unapaswa kurekebishwa ili kuwa wenye usawa na haki na unaoweza kuitikia vipaumbele na matarajio ya Afrika.

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: 251115517700/251115526373
Fax:251115518718/251115536950 Website: www.au.int

**Uanachama katika Vyama vya Kitaalamu** *(Orodha ya vyama vya kitaalamu ambavyo wewe ni mwanachama, taja nafasi yako pale inapohitajika)*

**Tawasifu ya uongozi :** *(Kwa maneno yasiyozidi mia tatu (300), toa muhtasari na vipengele muhimu vya ujuzi wako husika, uzoefu, malengo, na mafanikio)*

Nilihudumu kama Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Taifa la Kenya katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuanzia mwaka 2008 hadi 2013 ambapo niliongoza utekelezwaji wa majukumu ya serikali. Nikifanya kazi karibu na Rais Mwai Kibaki, nilitekeleza jukumu muhimu katika kuleta mageuzi ya kisiasa, kiuchumi, na mabadiliko katika sekta ya usalama, hususan katika kutunga Katiba ya Kenya ya 2010. Katika kipindi hicho, niliwakilisha Kenya katika mikutano ya ngazi za juu za mahusiano ya nje, nikitumia ujuzi wangu wa uongozi na diplomasia, katika jukwaa la kimataifa.

Nilichaguliwa kama Mbunge wa eneo bunge la Lang'ata jijini Nairobi mwaka wa 1992, nikahudumu kama mwakilishi wa eneo hilo kwa miaka 20. Wakati huu, pia nilihudumu kama Waziri wa Nishati chini ya Rais Daniel Arap Moi na Waziri wa Barabara, Ujenzi wa Umma na Makazi chini ya Rais Kibaki. Katika majukumu haya, niliongoza utekelezaji wa sera muhimu za serikali, nikilenga ufikiaji wa nishati, maendeleo ya miundombinu ya barabara, na kuboresha makazi duni, na kuweka msingi wa nyumba za bei nafuu. Zaidi ya hayo, nilipigania kupitishwa kwa sera za nishati safi, zikiwemo nishati ya jotoardhi na umeme wa maji.

Nikiwa Mwakilishi Mkuu wa AU kwa Maendeleo ya Miundombinu barani Afrika (2018 - 2023) kilinipa ufahamu muhimu kuhusu fursa na changamoto za miundombinu barani Afrika. Niliratibu utekelezaji wa PIDA, nikihamasisha uungwaji mkono kisiasa kutoka kwa Mataifa Wanachama na Jumuiya za Kikanda ili kukuza maendeleo ya miundombinu kote Afrika. Zaidi ya hayo, nilihamasisha uungwaji mkono kwa miradi ya bara na kukuza ushirikiano wa kikanda, nikizingatia utawala bora, utekelezwaji wa kistadi, na uwiano miongoni mwa wadau.

Ushiriki wangu mkubwa katika siasa za kitaifa za Kenya, kama kiongozi wa chama na mwanachama wa vyama vya muungano, umenijengea ujuzi wa kina wa sera za umma, na kunitunuku tuzo na heshima, ikiwa ni pamoja na tuzo la pili kuu nchini Kenya (Elder of the Order of the Golden Heart), Tuzo la Maslahi ya Wengi (Mizani Africa), Tuzo la Uongozi wa Kimataifa (BEFTTA), na Tuzo la huduma bora kwa wananchi, jamii na nchi kwa kipindi cha miaka hamsini (Golden Jubilee Award Kenya).

| |
|---|
| 2010 – Sasa: Mhandisi aliyesajiliwa, Bodi ya Usajili wa Wahandisi Kenya<br><br>2009 – Sasa: Mhandisi Mshirika, Chama cha Ujenzi wa Kenya<br><br>2002 – Sasa: Mshirika, Taasisi ya Wahandisi Kenya<br><br>1976 – 2002: Mwanachama, Taasisi ya Wahandisi Kenya |

**Tuzo za Kitaaluma na Kitaalamu** *(Onyesha tuzo zako za kitaaluma na kitaalamu, kwa kuanza na tuzo ya juu zaidi)*

| Jina la Taasisi | Anwani ya Taasisi (Anwani ya Posta, Namba za simu, na Tovuti) | Kiwango cha Kuhitimu | Mwaka wa Kuhitimu |
|---|---|---|---|
| *Chuo Kikuu cha Otto-Von-Guericke, Magdeburg, Ujerumani* | • Universitätspl. 2, 39106 Magdeburg, Ujerumani<br>• Simu: +49 391 6701<br>• Tovuti: https://www.ovgu.de/magdeburg | Shahada ya Uzamili ya Sayansi (Uhandisi wa Mitambo, Teknolojia ya Uzalishaji) | 1969 |
| *Taasisi ya Herder-Germany* | • Anwani: Frau Schröder Lumumbastraße 4, 04105 Leipzig<br>• Simu: +49 6421 1840<br>• Tovuti : https://www.herder-institut.de | Cheti cha Kidato cha Nne | 1964 |
| *Shule ya Msingi ya Kisumu Union & Shule ya Maranda* | • Anwani: 120 Bondo, Siaya, Kenya<br>• Simu: +254 799 914 034<br>• Tovuti : https://www.marandahighschool.sc.ke | Cheti cha Shule ya Msingi na Sekondari ya Msingi | 1962 |

**Mafunzo Mengine Muhimu** *(Onesha mafunzo/kozi zingine ulizohudhuria na kupewa cheti ambazo zinafaa kwa kazi hii)*

| Jina la Kozi | Taasisi Iliyotoa Cheti | Anwani ya Taasisi (Anwani ya Posta, Namba za simu, na Tovuti) | Mwaka Uliohudhuria |
|---|---|---|---|
| Cheti katika Usimamizi wa Juu | Taasis ya Usimamizi ya Kenyay (KIM) | Chuo cha Usimamizi ya Afrika<br>S.L.P – 43706-00100 Nairobi, Kenya<br><br>Simu: +254 712 200 969<br><br>Tovuti : https://www.kim.ac.ke | 1978 |
| Usimamizi wa ubora wa bidhaa na viwango | Chuo Kikuu cha Denver, Colorado, USA | Anwani: 2199 S. University Blvd, Denver, CO 80208, USA<br><br>Simu: +1 303 871 2000<br>Tovuti : https://www.du.edu | 1976 |
| Elimu kuhusu kuanzishwa kwa viwango vya kiasili | Ofisi ya Kitaifa ya Viwango na Teknolojia, Gaithersburg, MD., USA | *Anuani: 100 Bureau Drive, Gaithersburg, MD 20899, USA*<br><br>• Simu: +1 301 975 2000<br>• Tovuti : https://www.nist.gov | 1976 |
| Taasisi ya Mwongozo wa Viwango | Taasisi ya Viwango ya Uingereza , (BSI Group) | *Anuani: 389 Chiswick High Road, London, W4 4AL, Uingereza*<br><br>• Simu: 0345 086 9001<br>• Tovuti : https://www.bsigroup.com | 1975 |

**Uzoefu wa Kazi** *(Onesha uzoefu wako wa kazi kwa kuanza na kazi ya sasa au iliyopita hivi karibuni. Toa historia ya kina ya kazi na jumuisha/ inayoharirika ipasavyo ili kuonesha uzoefu wako wa kazi )*

**Jina la Shirika/ Mwajiri: Tume ya Muungano wa Afrika (AUC)**

**Anwani ya Shirika/Mwajiri (Anwani ya Posta, Namba za simu, na Tovuti):**

S.LP 3243, Roosvelt Street W21K19
Addis Ababa, Ethiopia.
Phone +251 115517700
Tovuti: https://www.au.int

| | |
|---|---|
| *Nafasi ya kazi (Jina la Kazi)* | **Mwakilishi Mkuu wa Maendeleo ya Miundombinu barani Afrika** |
| *Muda (Tarehe ya Kuanza na Tarehe ya Kumaliza)* | **2018-2023** |
| *Idadi ya Watu uliowasimamia* | **Wataalamu Wakuu Wanne (4)** |
| *Majukumu* | **A. Uzoefu katika Mashirika ya Muungano wa Afrika**<br><br>Nikiwa Mwakilishi Mkuu wa Maendeleo ya Miundombinu barani Afrika katika AU, nilipata uzoefu mkubwa katika mashirika ya AU. Nilifanya kazi kwa karibu na Mataifa Wanachama na mashirika mbalimbali ya AU kutekeleza miradi muhimu ya miundombinu chini ya PIDA. Jukumu langu lilihusu kutatua uhusiano mgumu kati ya Mataifa Wanachama wa AU, Mashirika ya AU, na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, kuhakikisha umoja na malengo ya mikakati na sera za AU. Majukumu muhimu chini ya wadhifa wangu yalikuwa:<br><br>i. Kuunga mkono juhudi za Shirika la Maendeleo ya Muungano wa Afrika - Mpango Mpya wa Maendeleo ya Afrika (AUDA - NEPAD) ndani ya mfumo wa PIDA, ambao Mkutano Mkuu wa AU uliidhinisha mwezi Januari, 2012.<br><br>ii. Kuhamasisha uungwaji mkono wa kisiasa kutoka kwa Mataifa Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda ili kurahisisha utekelezaji wa maendeleo ya miundombinu.<br><br>iii. Kushawishi wadau wa maendeleo kuunga mkono miradi mbalimbali ya Tume ya AU.<br><br>iv. Kufanya kazi na mpango maalum wa Marais teule wa kuendeleza miundombinu wa PIDA kuzingatia mahitaji ya kuboresha mtandao wa barabara barani Afrika.<br><br>v. Kufanikisha juhudi za kuwekatreni ya kasi barani, ambayo iko kwenye Miaka Kumi ya Kwanza ya utekelezaji wa Ajenda 2063 ya AU.<br><br>**B: Uongozi unaozingatia tofauti za kitamaduni barani Afrika**<br><br>Majukumu yangu ya uongozi kila mara yamehusu kusimamia watu tofauti tofauti katika tamaduni mbalimbali. Nikiwa Mwakilishi Mkuu wa Maendeleo ya Miundombinu barani Afrika, niliongoza jopo la wataalamu kutoka nchi mbalimbali za Afrika huku nikikuza mandhari ya ushirikiano unaozingatia tofauti za kitamaduni. Nina uzoefu mkubwa wa kuleta uwiano miongoni mwa wadau walio na usuli mbalimbali ili kuhakikisha kwamba miradi na sera zinaambatana na azimio za bara la Afrika. |

| | |
|---|---|
| *Mafanikio* | i. Kuhamasisha Mataifa Wanachama wa AU kutekeleza ramani ya miradi muhimu ya miundombinu ya bara;<br>ii. Kuchochea umiliki wa Afrika kwa miradi ya barabara kuu zinazounganisha bara;<br>iii. Kushinikiza kuharakishwa na uboreshaji wa mtandao wa barabara barani Afrika; na<br>iv. Kukuza miradi muhimu ya miundombinu, kupata msaada wa fedha kutoka kwa taasisi za kimataifa za fedha, na kuboresha uunganishaji wa kikanda. |
| **Jina la Shirika/Mwajiri: Serikali ya Jamhuri ya Taifa la Kenya** | |
| **Anwani ya Shirika/Mwajiri (Anwani ya Posta, Namba za simu, na Tovuti):**<br>Treasury Building, 14th Floor, Harambee Avenue<br>P.O. Box 74434,00200, Nairobi, Fax. 252299 | |
| *Nafasi ya Kazi (Jina la Kazi)* | **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kenya** |
| *Muda (Tarehe ya Kuanza na Tarehe ya Kumaliza)* | **2008-2013** |
| *Idadi ya Watu uliowasimamia* | **Mawaziri 42, Manaibu Mawaziri, na Makatibu Wakuu wa Wizara** |
| *Majukumu* | **A. Usimamizi wa Fedha**:<br><br>Kama Waziri Mkuu wa Kenya, nilikuwa na jukumu la kusimamia bajeti ya kitaifa na kutekeleza sera za kifedha zilizoboresha uwazi na ufanisi katika matumizi ya umma. Nilianzisha dhana ya mkataba wa utendajikazi serikalini, ambao uliimarisha sana uwajibikaji na usimamizi wa kifedha katika utoaji wa huduma za umma. Uzoefu wangu unajumuisha usimamizi wa bajeti kubwa, kuhakikisha usimamizi wa kifedha wenye busara, na kutekeleza mifumo inayoboresha uadilifu wa kifedha. Majukumu yangu muhimu yalikuwa:<br><br>i. Kuratibu na kusimamia Mawaziri wote, Manaibu Mawaziri, na Makatibu Wakuu wa Wizara;<br><br>ii. Kusimamia majukumu ya serikali ya kitaifa, kuongoza kamati za Baraza la Mawaziri, na kusimamia mageuzi ya utumishi wa umma;<br><br>iii. Kuratibu Kitengo cha Ufuatiliaji wa Ufanisi;<br><br>iv. Kusimamia Ukaguzi wa Mashirika ya Serikali; |

| | |
|---|---|
| | v. Kugawa au kuteua majukumu ya uratibu kwa Manaibu Waziri Mkuu;<br><br>vi. Kutoa taarifa kwa Bunge kuhusu utendaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu; na<br><br>vii. Kutekeleza majukumu mengine yoyote yaliyopewa na Rais wa Jamhuri ya Kenya.<br><br>**B. Mageuzi ya Teknolojia na Dijitali**<br><br>Kama Waziri Mkuu, nilisimamia utekelezaji wa Mipango ya Kenya ya Ruwaza ya 2030, ambayo ilijumuisha uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya mawasiliano na teknolojia.<br><br>**C. Uongozi wa Mashirika Makubwa**<br><br>Kama Waziri Mkuu, nilisimamia zaidi ya wizara 42, nikihakikisha utekelezaji kamilifu wa majukumu ya serikali. Jukumu langu lilijumuisha usimamizi wa kila siku, upangaji wa mkakati, na tathmini ya utendaji wa idara za serikali. |
| *Mafanikio* | i. Nilitekeleza jukumu muhimu katika kuanzisha na kusimamia serikali ya Umoja wa Kitaifa baada ya uchaguzi wa mwaka 2007;<br><br>ii. Niliweka nchi kwenye njia ya umoja wa kitaifa na maridhiano;<br><br>iii. Nilizingatia utawala wa kikatiba na uongozi wa kisheria;<br><br>iv. Niliimarisha ufufuzi na ukuaji wa uchumi<br><br>v. Nilianzisha dhana ya mkataba wa utendajikazi katika huduma za umma;<br><br>vi. Nilitekeleza jukumu muhimu katika kupatikana kwa Katiba ya mwaka 2010;<br><br>vii. Niliimarisha uhifadhi wa mazingira ya chimbuko za maji nchini Kenya, ikiwemo Msitu wa Mau; na<br><br>viii. Niliweka mifumo iliyoboresha usimamizi wa busara wa rasilimali za umma. |
| **Jina la Shirika/Mwajiri: Serikali ya Jamhuri ya Taifa la Kenya** | |
| **Anwani ya Shirika/Mwajiri (Anwani ya Posta, Namba za simu, na Tovuti):**<br>Wizara ya Ujenzi, Ngong Road,<br>S.L.P 30260, Nairobi | |

| SIMU: +254 723 101/ +254 723 188. | |
|---|---|
| *Nafasi ya Kazi (Jina la Kazi)* | **Waziri wa Barabara, na Ujenzi wa Nyumba** |
| *Muda (Tarehe ya Kuanza na Tarehe ya Kumaliza)* | **2003 - 2005** |
| *Idadi ya Watu uliowasimamia* | Maafisa wakuu kadhaa ikiwa ni pamoja na Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi Wakuu na Washauri. |
| *Majukumu* | 1. Uongozi na mwelekeo wa wizara<br>2. Kusimamia majukumu na taasisi muhimu zifuatazo:<br><br>i. Ujenzi an ukuzaji wa miundombinu ya barabara;<br><br>ii. Kazi za Ujenzi, upangaji na maendeleo ya sera, kuratibu ununuzi, viwango na ukuzaji wa miundombinu ya umma;<br><br>iii. Magari, ujenzi an uhifadhi wa majengo ya umma;<br><br>iv. Makazi na kuboresha/kuimarisha makazi duni;<br><br>v. Katibu Mkuu wa Kitaifa wa Makazi ya Binadamu vi. Kituo cha Utafiti wa Ujenzi cha Kenya;<br><br>vii. Kamati ya Kudhibiti Kodi;<br><br>viii. Usajili wa Wahandisi Wasanifu majengo na Wasanifu ramani.<br><br>ix. Usajili wa Wanakandarasi na Wauzaji wa Vifaa, vya ujenzi;<br><br>x. Shirika la Makazi la Kitaifa;<br><br>xi. Kampuni ya Fedha ya Nyumba ya Kenya; na<br><br>xii. Taasisi ya Kenya ya Teknolojia ya Barabara na Ujenzi wa Majengo. |
| *Mafanikio* | i. Nilianzisha Mipango ya Kenya ya Ruwaza ya 2030, nyaraka muhimu ya mpango wa Serikali ya Kenya;<br><br>ii. Nilizindua miradi ya makazi nafuu;<br><br>iii. Niliumba ramani ya kuboresha makazi ya mitaa duni; |

| | |
|---|---|
| | iv. Nilirejesha ardhi ya umma kwa matumizi ya umma; na<br><br>v. Niliongoza ujenzi na uboreshaji wa mtandao wa barabara nchini Kenya ikiwa ni pamoja na barabara za kimataifa. |
| **Jina la Shirika/Mwajiri: Serikali ya Jamhuri ya Taifa la Kenya** | |
| **Anuani ya Shirika/Mwajiri (Anwani ya Posta, Namba za simu, na Tovuti):**<br>Nyayo House, Kenyatta Avenue,<br>P.O. Box 30582, Nairobi.<br>Telephone: +254 20 4841000<br>Tovuti: https://www.energy.go.ke | |
| *Nafasi ya Kazi (Jina la Kazi)* | Waziri wa Kawi |
| *Muda (Tarehe ya Kuanza na Tarehe ya Kumaliza)* | **2001 - 2002** |
| *Idadi ya Watu uliowasimamia* | Maafisa wakuu kadhaa ikiwa ni pamoja na Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi Watendaji na Washauri. |
| *Majukumu* | Nilisimamia majukumu muhimu yafuatayo katika kuendeleza Programu na Mashirika ya Serikali:<br><br>i. Maendeleo ya sera ya kawi;<br>ii. Maendeleo ya umeme wa maji;<br>iii. Utafutaji na maendeleo ya nishati ya joto ardhi;<br>iv. Maendeleo ya umeme wa joto moto;<br>v. Sera ya bidhaa za mafutauagizaji /mauzo<br>vi. Maendeleo ya nishati mbadala;<br>vii. Udhibiti wa nishati, usalama na uhifadhi;<br>viii. Utafutaji na maendeleo ya mafuta ya asili;<br>ix. Kampuni ya Usambazaji wa Umeme nchini Kenya;<br>x. Mpango wa Umeme Vijijini;<br>xi. Kampuni ya Kuchakata Petroli ya Kenya;<br>xii. Kampuni ya Uzalishaji wa Umeme nchini Kenya;<br>xiii. Shirika la Kitaifa la Mafuta ya Kenya;<br>xiv. Kampuni ya Bomba la Mafuta ya Kenya;<br>xv. Tume ya Udhibiti wa Nishati; na<br>xvi. Mamlaka ya Umeme Vijijini. |
| *Mafanikio* | i. Nilirekebisha sekta ya nishati;<br>ii. Niliendeleza nishati ya kijani;<br>iii. Niliimarisha upanuzi wa umeme vijijini; na<br>iv. Niliimarisha uwajibikaji na ufanisi katika sekta ya nishati. |
| **Jina la Shirika/Mwajiri : Bunge la Taifa la Kenya** | |
| **Anwani ya Shirika/Mwajiri (Anwani ya Posta, Namba za simu, na Tovuti):** | |

| | |
|---|---|
| The Clerk, National Assembly<br>Simu: 254 2 2221291 or 2848000<br>Tovuti: https://www.parliament.go.ke | |
| *Nafasi ya Kazi (Jina la Kazi)* | **Mbunge wa eneobunge la Langata** |
| *Muda (Tarehe ya Kuanza na Tarehe ya Kumaliza)* | 1992 - 2013 |
| *Idadi ya Watu uliowasimamia* | **Niliwakilisha wakaazi takriban 335,000** |
| *Majukumu* | i. Kutunga sheria;<br>ii. Kuwakilisha wananchi wa eneobunge la Langata;<br>iii. Kusimamia Serikali;<br>iv. Kutenga fedha kwa matumizi; na<br>v. Uamuzi na mgawo wa mapato ya kitaifa. |
| *Mafanikio* | i. Nilitunga sheria, niliwakilisha wapiga kura, na kufanya usimamizi wa serikali;<br>ii. Waziri mbadala wa Serikali ya Mitaa<br>iii. Niliandaa marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa;<br>iv. Kuwa Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Bunge kuhusu kuanzishwa kwa Tume ya Mapitio ya Katiba ya Kenya (CKRC), iliyoandika Katiba ya Kenya ya 2010;<br>v. Niliteua wajumbe wa CKRC; na<br>vi. Nilianzisha makazi nafuu; kuimarisha upatikanaji wa usafiri wa umma; kukuza ujenzi wa shule, vituo vya afya; na usalama wa kudumu kwa ushirikiano na jamii. |
| **Jina la Shirika/Mwajiri: Shirika la ukaguzi na ubora wa bidhaa** | |
| **Anwani ya Shirika/Mwajiri (Anwani ya Posta, Namba za simu, na Tovuti):**<br>S.L.P 54974-00200, Nairobi.<br>Simu: +254 20 6948000<br>Tovuti: https://www.kebs.org | |
| *Nafasi ya Kazi (Jina la Kazi)* | **Naibu Mkurugenzi** |
| *Muda (Tarehe ya Kuanza na Tarehe ya Kumaliza)* | **1978- 1982 Naibu Mkurugenzi**<br>**1975-1978 (Mkurugenzi wa Viwango, Mhandisi)** |
| *Idadi ya Watu uliowasimamia* | Mameneja wakuu ishirini (20) |
| *Majukumu* | i. Kuongoza maendeleo na utekelezaji wa Viwango vya Ubora kwa Serikali ya Kenya (Mizani, Joto, Urefu na Kiasi) |

| | |
|---|---|
| | ii. Mafunzo na uongozi wa mafundi maabara wa mizani. |
| *Mafanikio* | i. Niliongoza kuanzishwa kwa Shirika la Viwango vya Ubora la Kenya (KEBS)<br>ii. Nilikuza Viwango vya Ubora wa viwango kwa Kenya (Mizani, Joto, Urefu na Kiasi). |
| **Jina la Shirika/Mwajiri: Chuo Kikuu cha Nairobi** | |
| **Anwani ya Shirika/Mwajiri (Anwani ya Posta, Namba za simu, na Tovuti):**<br>S.L.P 30197 – 00100, Nairobi.<br>Simu: +254 20 4910000<br>Tovuti : https://www.uonbi.ac.ke | |
| *Nafasi ya Kazi (Jina la Kazi)* | **Mhadhiri** |
| *Muda (Tarehe ya Kuanza na Tarehe ya Kumaliza)* | 1970-1973 |
| *Idadi ya Watu uliowasimamia* | Wanafunzi 120 |
| *Majukumu* | Kufundisha Uhandisi wa Makanika (Teknolojia ya Uzalishaji na Sayansi) |
| *Mafanikio* | Kufundisha, kushauri na kufuzu wanafunzi. |

**Ujuzi na Umahiri** *(Kwa maneno yasiyozidi mia tano (500), onesha jinsi uzoefu wako na sifa zako zinavyoendana na ujuzi na uwezo ulioainishwa katika maelezo ya kazi ya nafasi unayoomba)*

Nina ujuzi mkubwa wa kidiplomasia na uwezo wa kutetea haki na masuala ya kijamii ambao umedhihirika, nikiwa na uwezo wa kushirikiana na viongozi wa kimataifa, bara, na kikanda kwa lengo la kukuza maslahi ya Afrika. Nina imani kubwa kwamba ujuzi na uwezo wangu uliofafanuliwa hapa chini unaniweka kufaa zaidi kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Tume ya Muungano wa Afrika:

1. **Uzoefu katika Muungano wa Afrika**: Kama Mwakilishi Mkuu wa Muungano wa Afrika kwa Maendeleo ya Miundombinu barani Afrika, nilipata uzoefu mkubwa katika Muungano wa Afrika. Nilishirikiana kwa karibu na nchi wanachama na taasisi za Muungano wa Afrika kuunda na kutekeleza miradi muhimu ya miundombinu chini ya PIDA. Majukumu yangu yalihusisha kutatua mizozo na mahusiano kati ya Muungano wa Afrika, nchi wanachamajumuia za kikanda, na washirika muhimu huku nikihakikisha kwamba malengo muhumu ya Muungano wa Afrika yanatimika.

2. **Uongozi wa Mashirika Makubwa**: Katika kazi zangu zote, nimedhihirisha uwezo wa kusimamia mashirika makubwa kwa ufanisi. Kama Waziri Mkuu, nilisimamia zaidi ya wizara arobaini na mbili (42), na kuhakikisha utekelezaji mufti wa majukumu ya serikali. Majukumu yangu yalijumuisha usimamizi wa kila siku, upangaji mkakati, na tathmini ya utendaji wa idara za serikali. Vivyo hivyo, katika Muungano wa Afrika, niliongoza timu ya washauri wakuu, nikiratibu juhudi katika miradi mingi ya asasi tofauti tofauti kutekeleza miradi za Tume ya AU.

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: 251115517700/251115526373
Fax:251115518718/251115536950 Website: www.au.int

3. Hadhi ya Kimataifa: Nimewakilisha nchi yangu na bara langu katika majukwaa makubwa ya kimataifa ikiwemo kama mpatanishi wa amani na msimamizi wa uchaguzi, na kwa hivyo nikapata ujuzi na uzoefu mwafaka wa kuwakilisha bara la Afrika.

4. **Utaalamu wa Usimamizi wa Fedha**: Katika kipindi changu kama Waziri Mkuu wa Kenya, nilikuwa na jukumu la kusimamia bajeti ya kitaifa na kutekeleza sera za kifedha zilizoboresha uwazi na ufanisi katika matumizi ya umma. Nilianzisha mfumo wa mikataba ya utendajikazi serikalini, ambao uliboresha sana uwajibikaji na usimamizi wa kifedha katika utoaji huduma za umma.

5. **Uongozi unaozingatia tofauti za kitamaduni barani**: Nafasi zangu za uongozi zimejumuisha kusimamia na kuongoza timu za watu wenye tamaduni na mazingira ya kisiasa tofauti. Kama kiongozi wa kitaifa nchini Kenya, nilitekeleza wajibu mkubwa katika uundaji na usimamizi wa serikali ya muungano wenye maslahi ya kisiasa yanayopingana. Kama Mwakilishi Mkuu wa Muungano wa Afrika kwa Maendeleo ya Miundombinu, niliongoza timu ya washauri kutoka nchi mbalimbali za Afrika, nikiimarisha mazingira ya ushirikiano unaotumia fursa ya tofauti za kitamaduni na kisiasa. Nina historia thabiti ya kutetea wasio na uwezo, kuleta uwiano miongoni mwa wadau kutoka maeneo mbalimbali, kuhakikisha kuwa sera na miradi yanaakisi matamanio ya Waafrika.

6. **Ufundi na Mageuzi ya Kidijitali:** Nimekuwa mstari wa mbele katika kusukuma ushawishi wa teknolojia katika nyanja mbalimbali za kazi yangu. Kama Waziri Mkuu, nilisimamia utekelezaji wa Mipango ya Kenya ya Ruwaza ya 2030, ambayo ilijumuisha uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya mawasiliano na teknolojia. Aidha, katika nafasi yangu katika Muungano wa Afrika, nilisaidia kuhamasisha matumizi ya suluhisho za kidijitali katika miradi ya miundombinu, kama vile reli ya kasi ya bara na miradi ya miji ya kisasa.

**Mafanikio:** *(Kwa maneno yasiyozidi mia tano (500), onesha mafanikio mengine yoyote zaidi ya yale yaliyo chini ya uzoefu wa kazi ambayo ungependa kuyasisitizia )*

**A. Upatanishi wa Amani**

i. 2018: Niliongoza juhudi za kuleta amani Sudan Kusini.

ii. 2010-2011: Mpatanishi Mkuu wa Muungano wa Afrika kusuluhisha mgogoro wa kisiasa nchini Ivory Coast baada ya uchaguzi wa urais wa 2010.

iii. 1996: Nilifanya kazi na Rais Mwalimu Julius Nyerere katika kuleta amani Burundi.

iv. Miaka ya 1990: Nilifanya kazi kwa karibu na International Republican Institute kuleta amani Msumbiji.

**B. Uchaguzi na Utawala Bora**

i. Nilifanya kazi na International Republican Institute kutoa mafunzo kwa vyama vya kisiasa Zimbabwe.
ii. Nilihudumu kama msimamizi wa uchaguzi katika nchi kadhaa, ikiwa ni pamoja na Nigeria, Msumbiji, na Lesotho.

**C. Maendeleo, Biashara na Ujasiriamali**

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: 251115517700/251115526373
Fax:251115518718/251115536950 Website: www.au.int

i. 2023: Mikutano ya ngazi ya juu na viongozi wa Afrika Kusini kutoka serikalini, mashirika yasiyo ya kiserikali, na sekta ya biashara pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo la Muungano wa Afrika (AUDA-NEPAD), kuchambua maendeleo ya Mpango wa Hatua ya Kipaumbele 2 wa Programu ya Maendeleo ya Miundombinu Afrika.

ii. 2022: Msemaji, Miundombinu Iliyo Imara Dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi, kongamano la 27 la Vyama vya Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP 27), Sharm El Sheikh, Misri

iii. 2022: Hotuba, "Kuiweka Afrika kwenye Misingi Imara kwa Ajili ya Kurejesha, Ukuaji, na Uimara kupitia Miundombinu" Programu ya Maendeleo ya Miundombinu Afrika (PIDA), Nairobi, Kenya.

iv. 2018: Mashauriano ya ngazi ya juu na Waziri Mkuu Narendra Modi wa India kuhusu uhusiano wa biashara kati ya India na Kenya.

v. 2011: Mshiriki katika kongamano la "Ushirikiano kuu wa Kawi", Ushirikiano wa Ufadhili wa Kawi, Oslo, Norway.

vi. 2011: Mshiriki katika kongamano la "Ushirikiano kuu wa Kawi", Ushirikiano wa Ufadhili wa Kawi, Copenhagen, Denmark.

vii. 2010: Mshiriki katika Kongamano la 16 la Vyama vya Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP 16) Cancun, Mexico.

viii. 2009: Mshiriki katika Kongamano la 15 la Vyama vya Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP 15), Copenhagen, Denmark.

xi. Mwanzilishi na mjasiriamali, East Africa Spectre, mtengenezaji wa silinda za gesi kwa Kenya na kanda ya Afrika Mashariki.

**Machapisho (Kama yapo):** *(Orodhesha machapisho ambayo umeandika au kuandika kwa pamoja na mwandishi mwingine, toa viungo vya kufikia machapisho hayo kama yapo mtandaoni)*

i. Raila Amolo Odinga, THE QUEST FOR NATIONHOOD: ROADMAP TO OUR FUTURE (Nairobi: Mountaintop Publishers, 2017).

ii. Raila Amolo Odinga, RAILA ODINGA: THE FLAME OF FREEDOM (Nairobi: Mountaintop Publishers, 2013).

**TUZO MBALIMBALI ZA HADHI**

i. Mei 2021: Tuzo la Greater Good, Mizani Africa, Nairobi, Kenya

ii. Desemba 2018: Daktari wa Sayansi (Honoris Causa), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga, Siaya, Kenya

iii. Mei 2018: Tuzo la BEFFTA kwa Uongozi wa Kimataifa (The Black Entertainment Film Fashion Television and

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: 251115517700/251115526373
Fax:251115518718/251115536950 Website: www.au.int

Arts), London, UK

iv. Machi 2018: Tuzo la juhudi za uwiano na maridhiano nchini Kenya (Embrace Women, Building Bridges in Kenya)

v. Desemba 2013: Tuzo la huduma bora kwa wananchi, jamii na nchi kwa kipindi cha miaka hamsini (Golden Jubilee Award Kenya), iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Kenya

vi. Mei 2012: Shahada ya Uongozi katika Maendeleo ya Jamii (Honoris Causa), Chuo Kikuu cha Teknolojia ya Ubunifu cha Limkokwing, Kuala Lumpur

vii. 2010: Daktari wa Barua (Honoris Causa), Chuo Kikuu cha Maseno, Kenya

viii. 2009: Shahada ya Heshima, Chuo Kikuu cha Kilimo na Makanika cha Florida, USA

ix. Oktoba 2008: Shahada ya Sheria (LLD) (Honoris Causa), Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya

x. 2008: Tuzo la pili kuu nchini Kenya (Elder of the Order of the Golden Heart) , aliyetunukiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Kenya

**Lugha za Kazi** ***(Onesha viwango vyako vya ustadi wa kuongea, kusoma, na kuandika lugha za AU zilizoorodheshwa hapa chini. Mifano ya viwango vya ustadi: Nzuri sana, Nzuri, Kawaida, au Mbaya)***

| Lugha za Kazi | Kuongea | Kusoma | Kuandika |
|---|---|---|---|
| Kiarabu | | | |
| Kiingereza | Ana umilisi mzuri | Ana umilisi mzuri | Ana umilisi mzuri |
| Kifaransa | | | |
| Kireno | | | |
| Kiswahili | Ana umilisi mzuri | Ana umilisi mzuri | Ana umilisi mzuri |

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: 251115517700/251115526373
Fax:251115518718/251115536950 Website: www.au.int

**Wadhamini** *(Onesha watu watatu ambao ni wadhamini wako kwa kutumia maelezo ya hapa chini. Mdhamini mmoja anapaswa kuwa mdhamini anayekufahamu kikazi na mmoja awe mdhamini anayekufahamu nje ya kazi)*

| Jina | Kazi na Shirika | Barua pepe | Namba ya Simu |
|---|---|---|---|
| 1. Eng. Meschack Kidenda | Aliyekuwa Mkurugenzi Mamlaka ya Kitaifa ya Barabara kuu ya Kenya | | |
| 2. H.E Dr. Graca Machel | Mwanamke Mashuhuri barani Afrika | | |
| 3. H.E Olesegun Obasanjo | Aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Nigeria | | |

**Uthibitisho**

*Mimi, niliyesaini hapa chini, nathibitisha kuwa taarifa hii inanielezea mimi kiusahihi, sifa zangu, na uzoefu wangu.*

| | |
|---|---|
| **Jina** | Raila Amolo Odinga |
| **Saini** | [signature] |
| **Tarehe** | 27/07/2024. |